

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA MTWARA

Simu Na: 023 2410030

Nukushi: 023 2410030

Baruapepe: ded@tandahimbadc.go.tz

Tovuti: www.tandahimbadc.go.tz

Unapojibu taafadhali taja



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 03,

TANDAHIMBA.

Kumb. Na. JB.124/294/01A/85

11 Novemba, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kuleta maombi ya kazi kwa nafasi zilizoainishwa hapo chini, baada ya kupata kibali cha ajira mbadala chenye Kumbu. Na .FA. 170/362/01"B"/15 cha tarehe 15 Octoba, 2021, kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira mpya. Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Tandahimba anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi husika.

MTENDAJI WA KIJIKI III (NAFASI 5)

i. Sifa za Kitaaluma kwa mwombaji.

a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)au Sita (VI).

b) Awe amepata mafunzo ya stadi ya kazi ngazi ya cheti katika fani zifuatazo;Utawala, Sheria ,Rasilimali watu,Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Sanaa

kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au vyuo vingine vinavyoambuliwa na Serikali.

ii. Mshahara

Ngazi ya mshahara **TGS B1** (Mshahara kwa mwezi Tsh. 390,000/=)

iii. Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji III

- a) Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- b) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- c) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri.
- d) Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
- e) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini, na kuongeza uzalishaji mali.
- f) Kusimamia na kuratibu upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya jamii.
- g) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
- h) Kusimamia, Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote za nyaraka za Kijiji.
- i) Mwenyekiti wa Kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji.
- j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- k) Atawajibuka kwa Mtendaji wa Kata.


MASHARTI YA JUMLA YA MAOMBAJI WA NAFASI ZA KAZI

- a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania mwenye Umri kuanzia miaka 18 na wasizidi umri wa miaka 45.
- b) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi kijiji chochote kile ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
- c) Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- d) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma , Kidato cha Nne na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.

- e) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- f) Waombaji waambatanishe na picha ndogo 2 pasport size zilizopigwa hivi karibuni.
- g) "Testimonials", "*provisional results*", "*statement of results*", Hati ya matokeo ya Kidato cha nne "*result slip*" **havitakubaliwa.**
- h) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha Nne na Cheti cha Taaluma ambao vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).
- i) Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa au kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi.
- j) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- k) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- l) Uwasilishaji wa taarifa za kugushi utaadhibiwa kisheria; aidha, maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Masjala ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba au kutumwa kupitia posta kwa anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 03,
TANDAHIMBA – MTWARA.**

j) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 26/11/2021 saa 09:30 Alasiri.


Mussa L. Gama
Mkurugenzi Mtendaji (W),
TANDAHIMBA